

WATUNZA KUMBUKUMBU NA MAAFISA RASILIMALIWATU WATAKIWA KUZINGATIA UADILIFU KATIKA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA SERIKALI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Taaluma Na. 1,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
18 Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
40404 DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

WATUNZA KUMBUKUMBU NA MAAFISA RASILIMALIWATU WATAKIWA KUZINGATIA UADILIFU KATIKA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA SERIKALI

Serikali imewataka Watunza Kumbukumbu na Maafisa Rasilimaliwatu kuhakikisha kumbukumbu na nyaraka zinatunzwa vizuri kwa kuzingatia uadilifu, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayotolewa na Serikali ili kurahisisha utendaji kazi.

Hayo yamesemwa na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Francis Michael alipokuwa akifungua kikao kazi cha siku tatu cha Watunza Kumbukumbu na Maafisa Rasilimaliwatu Serikalini chenye lengo la kujadili masuala ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika Utumishi wa Umma kilichoanza leo jijini Dodoma.

Dkt. Michael amesema, uadilifu katika kutekeleza majukumu yetu ni jambo la msingi sana hivyo kwa wale ambao si waadilifu wabadilike ili tuweze kuwa na mchango katika kujenga utumishi wa umma uliotukuka.

Dkt. Michael amefafanua kuwa, kukosekana kwa taarifa sahihi na kwa wakati kunaweza kufanya Watendaji wa Serikali kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kusababisha ucheleweshwaji wa maamuzi au kutolewa kwa maamuzi yasiyo sahihi na yasiyokidhi matarajio ya wananchi.

"Kutotunza vizuri kumbukumbu na nyaraka, mianya ya rushwa, ubadhirifu wa mali za umma na matumizi mabaya ya madaraka kunachangia sana kuzorotesha maendeleo ya uchumi wa Taifa." Dkt. Michael ameongeza.

Sanjari na hayo, Dkt. Michael ameipongeza Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa kwa kuandaa kikao kazi hicho na ameitaka Idara hiyo kuhakikisha kinakuwa endelevu ili kuongeza elimu ya utunzaji

kumbukumbu ambao kwasasa unalenga kuboresha uendeshaji wa Masijala kutoka kwenye mfumo wa kawaida kuwa wa kielektroniki.

Aidha, Dkt. Michael amesema Serikali itaendelea kuzifanyia kazi changamoto mbalimbali za kada ya Watunza Kumbukumbu kadri zinavyojitokeza ili kuboresha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali.

Naye Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Bw. Firimin Msiangi ameahidi kufanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na Naibu Katibu Mkuu ili utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika taasisi za umma uwe na manufaa katika utendaji kazi wa taasisi na kwa maendeleo ya taifa.

Bw. Msiangi amesema kikao kazi hicho kimeongozwa na Kauli Mbiu isemayo ni "Utoaji wa Huduma za Masijala katika Mifumo ya Kielektroniki:Wajibu wetu na Utunzaji bora wa Kumbukumbu katika kuimarisha utoaji huduma Serikalini."

Mada zinazojadiliwa ni pamoja na Utunzaji na Utumiaji wa Kumbukumbu katika Utumishi wa Umma, Kumbukumbu za Mahakama na Umuhimu wake katika Kutenda Haki kwa Wakati, Matumizi ya TEHAMA katika Uendeshaji wa Masijali za Serikali.

Mada nyingine ni Wajibu, Usalama na Usimamizi wa Utunzaji Kumbukumbu Tuli katika Taasisi za Umma, Ukusanyaji wa Nyaraka kutoka Taasisi za Umma katika Kuhifadhi Historia na Urithi Andishi wa Taifa letu na Uzingativu wa Maadili katika Utunzaji wa Kumbukumbu na Taaifa za Serikali.

Kikao kazi hicho kimeandaliwa na Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa na kimeshirikisha Watunza Kumbukumbu na Maafisa Rasilimaliwatu kutoka taasisi mbalimbali za Serikali.

IMETOLEWA NA;
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
OFISI YA RAIS (UTUMISHI)
TAREHE 25 JUNI, 2019